**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

BUNGE LA TANZANIA

---

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

---

Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
**DODOMA.**

**APRILI, 2020**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

Kifungu cha 6 (4)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kinatoa wajibu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti ambalo hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, hutanguliwa na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Singida na

Manyara, iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020 kuanzia tarehe 11 hadi 15 Machi, 2020. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 16 na 17 Machi, 2020.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Mafungu Nane (8) ya bajeti kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;
iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na
viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa Fedha 2020/2021; na
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais , Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa kiasi cha Tsh **198,389,120,525/**= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu manne (4) kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Tshs **154,189,384,717/=;**

ii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Tshs**. 41,060,000,000/=;**

iii) **Fungu 33**: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – Tshs. **1,139,735,808/=;** na

iv) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – Tshs.**2,000,000,000/=.**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi iliyotembelewa inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Mradi Na.6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 76,626,997,721/= na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mfuko huu ambao unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, uko katika sehemu ya pili ya utekelezaji wa awamu ya tatu ambayo umejikita katika kuzitambua kaya maskini kwenye Vijiji/Mitaa/Shehia zilizosalia kwa lengo la kuzisaidia kujimudu kiuchumi kwa kupunguza umaskini wa kipato; kuboresha maisha na ustawi wa jamii; na kushawishi wananchi kuwajibika katika ufanyaji wa kazi.

Taarifa ya Utekelezaji inaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 TASAF iliweza kutoa ruzuku ya **shilingi bilioni 35.6** kwa kaya maskini **992,526** zilizoandikishwa zenye jumla ya watu **Milioni 5.2** kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar katika Vijiji/Mitaa/Shehia **9,867.** Kaya hizo zilipata ruzuku hiyo kwa kuzingatia masharti ya lishe, afya na elimu.

Aidha, katika kipindi hicho kulikuwa na utekelezaji wa miradi 1,521 katika Vijiji,Mitaa na Shehia zipatazo 1,212 ambao uliwezesha kaya 161,416 kupata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar.

Miradi hiyo ambayo iligharimu **shilingi bilioni 6.4** ilihusu ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji; uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti; uchimbaji wa visima vifupi; uboreshaji wa barabara; uhifadhi wa vyanzo vya maji na hifadhi za mazingira.

Vilevile, TASAF iliandaa mfumo wa malipo kwa walengwa kwa njia ya kielektroniki kupitia mitandao ya simu na benki na kufanyiwa majaribio

katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji **16** za Tanzania Bara**.** Baadhi ya maeneo hayo ni Jiji la Arusha, Manispaa ya Ilala, Manispaa ya Temeke, Halmashauri ya Bahi, Mpanda Mji, Halmashauri ya Siha, Halmashauri ya Kisarawe, Manispaa ya Kigoma – Ujiji; Manispaa ya Songea; Halmashauri ya Urambo na Halmashauri ya Muheza. Aidha, Halmashauri zote za Unguja na Zanzibar zilihusishwa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 jumla ya Walengwa **55,087** walipokea malipo yenye thamani ya **shilingi bilioni 2.14** kwa njia hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mpango huu Kamati ilitembelea na kukagua Mtaa wa Sokoine Manispaa ya Singida, na Mkoa wa Manyara.

### 2.1.2 Na.4921 – Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 1,500,000,000/= na unatekelezwa chini ya Kifungu **1003** kiitwacho '***Policy and planing***' cha **Fungu 30 –** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mpango huu unatekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Mpango huu umewezesha wanyonge kurasimisha ardhi na biashara na kuvitumia kukuza mitaji ya shughuli za kiuchumi.

Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilibainisha kuwa, Wakulima **180** na Viongozi **22** wa vyama vya wakulima wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi zingine za Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Aidha, mafunzo hayo yamewezesha Wakulima 48 katika Vijiji vya Mvumi na Magubike kufungua Akaunti katika Benki.

Aidha, huduma za urasimishaji wa biashara zimesongezwa kwa wananchi kwa kuanzisha vituo vya pamoja (**One Stop Business Formalization and Development Centre)** katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Mji wa Babati ambapo huduma muhimu hutolewa kama leseni za biashara, utoaji wa namba ya utambulisho wa mlipa kodi **(TIN)** kupitia **TRA**, usajili wa jina la biashara kupitia **BRELA**, huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Aidha, Wafanyabiashara **1,529** wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara katika kipindi husika Vituo vimesajiliwa biashara **313** na Wafanyabiashara 420 wamefunga akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kujiongezea mitaji.

Vilevile, zoezi la urasimishaji wa ardhi mijini kwa dhana ya Mfuko Endelevu wa Wilaya limeanza kwa kufanya utambuzi wa milki **200** kati ya **1,000** zilizopangwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Mkoani Singida ili kujiridhisha kuhusu shughuli zinazotekelezwa na MKURABITA.

### 2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** chuo hiki kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinaendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu, na kutoa kozi za kitaaluma kwa ngazi za astashahada, stashahada na shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Raslimali Watu, Utawala na Manunuzi ya Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo kupitia Kampasi Sita (6) za Dar es Salam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya.

Aidha, utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma umeendelea kuimarishwa ili kuwajengea uwezo katika utendaji kazi na kutoa

huduma bora kwa wananchi. Hili limeimarishwa zaidi baada ya iliyokuwa Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao **(TaGLA**) kuunganishwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kupitia Tangazo la Serikali **Na.63** la Tarehe 31 Januari, 2020.

Ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kampasi ya Singida ili kukagua utekelezaji wa chuo hicho pamoja na eneo la Mungumaji ambako majengo ya Kampasi hiyo yanatarajiwa kujengwa.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo hiyo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka wa fedha 2019/2020 naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tufuku kuhusu mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo: -

### 2.2.1. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini 'Support to Tanzania Social Action Fundi'

i. **Mheshimwa Spika**, katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Kamati ilitembelea na kukagua Mtaa wa Sokoine ambao una jumla ya kaya **2,824** zinazonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini ambapo hadi Februari,2020 jumla ya shilingi bilioni **4.2** zilikuwa zimepelekwa kwa ajili ya ruzuku za msingi na utekelezaji wa shughuli zingine.

Manispaa ya Singida ni miongoni wa Halmashauri 10 za Tanzania zinazotekeleza Mpango wa Timiza Malengo wa kuwezesha wasichana balehe na wanawake vijana kutimiza malengo kielimu na kufikia ndoto zao **(Adolescent Girls and Young women – AGYW**) unaofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii **(TASAF**) kwa kushirikiana na Tume ya

kudhibiti UKIMWI **(TACAIDS**). Halmashauri nyingine zinazotekeleza mpango huu ni Kongwa, Mpwapwa, Bahi, Kilombero, Ulanga, Kondoa Mji na Ifakara Mji.

Mpango wa **AGYW** unawahusu wasichana wote walio kwenye kaya zilizo kwenye mpango wa TASAF wa kunusuru kaya maskini katika Manispaa ya Singida na ulianza Juni, 2018 kwa kufanya utambuzi wa kuwatambua wasichana hao kutoka kaya zinazonufaika. Katika utambuzi huo jumla ya wasichana **2,250** walitambuliwa na kati ya hao **1,303** wanasoma katika shule mbalimbali na **947** hawasomi.

Utekelezaji wa Mpango wa Timiza Malengo **(AGYW)** uko katika maeneo mawili; utoaji wa ruzuku kwa wasichana balehe waliopo shuleni, na kwa wanawake vijana waliokosa fursa ya shule kwa kuendesha shughuli zao kwa kwa lengo la kukuza kipato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata ushuhuda kutoka mnufaika wa ruzuku ya kaya maskini Bi. Edith Brayson Makala (miaka 55) ambaye anaishi katika Mtaa wa Sokoine ambaye ameamua kuitumia vyema kauli mbiu ya "Hapa Kazi tu" ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambayo imemuwezesha kuinua uchumi wa familia yake kupitia ruzuku ya kaya maskini kutoka **TASAF.**

**Bi. Makala** alianza kwa ajira ya muda chini ya mpango wa kunusuru kaya maskini mwaka 2016 ambapo alifanya kwa miezi minne (4) na kupata kipato kilichomuwezesha kununua cherehani na kuanza kujishughulisha na ushonaji, huku akimpatia mume wake mtaji wa biashara ya maji.

Mwaka 2018 alipata tena ajira ya muda ambayo ilimuwezesha kununua cherehani ya pili na hivyo kuongeza shughuli za ushonaji kwa kushirikiana na binti yake. Vyerehani hivyo vyenye

thamani ya shilingi 400,000/= vinamuwezesha Bi. Makala kuendesha shughuli za ushonaji wa nguo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sare za shule na mashuka.

*"Tumejikita kushona sare za shule kwani ni biashara endelevu kwa kuwa watoto wanasoma kila siku na kila mwaka, hivyo itasaidia kuboresha maisha yangu na familia."* Alisema Bi. Makala na kuongeza kwamba, kipato anachokipata kimemuwezesha kusomesha watoto wake sekondari na mmoja amefikia elimu ya chuo kikuu.

**Mheshimiwa Spika**, mnufaika mwingine ni Bi. Ester Ikumbi ambaye alijikuta katika maisha magumu sana baada ya kutelekezwa na mume wake akiwa na watoto watano (5). Anaeleza kwamba, alifanya kazi katika ajira za muda za wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini na kupata kipato kilichomuwezesha kuboresha hali yake ya kiuchumi hadi kufikia hatua ya kununua kiwanja na kuanza ujenzi wa nyumba.

**"***Ninamshukuru sana Rais Magufuli kwa TASAF kwani imenirejeshea tumaini la kuishi, mimi na watoto wangu. Nilikuwa nimekata tama kabisa, lakini sasa nafurahia maisha."* Anasema Bi. Ikumbi na kuongeza kwamba, ameingia katika ujasiriamali kwa kuanzisha utengenezaji wa sabuni za maji na batiki ili kukuza kipato kitakachomuwezesha kulea na kusomesha watoto wake.

**ii.** **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kujionea utekelezaji wa Mpango wa kunusuru Kaya masikini katika Halmashauri ya Mji wa Babati, ambao ulianza mwaka 2015 kwa kutambua na kuandikisha jumla ya Kaya **1,439.** Hata hivyo, baada ya uhakiki kwa lengo la kubaini na kuondoa kaya zisizo na sifa kaya hizo zilipungua hadi kaya **1,115.** Hadi kufikia Februari, 2020 malipo

ya ruzuku yalikuwa yamefanyika kwa awamu 23 ambapo jumla ya **shilingi milioni 977.7** zimetumika kwa ajili ya uhawilishaji fedha kwa kaya masikini.

Utekelezaji wa mpango huu umesaidia kuboresha hali ya maisha kwa wanufaika kwa kuwawezesha kupata mlo wa uhakika, watoto kutoka kaya za wanufaika kuhudhuria masomo na wale walio chini ya miaka mitano kuhudhuria kliniki kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mtaa wa Mrara uliopo kata ya Babati na kukutana na wanufaika wawili ambao kupitia ajira za muda zinazotolewa na mpango wa TASAF wameweza kuboresha maisha yao kwa kujiongezea kipato.

Bi. Albina Mathayo ambaye ni mjane aliyefanya kazi katika ajira za muda na kupata mtaji ambao umemuwezesha kuanzisha mradi wa kupasua kokoto, na ufugaji wa mbuzi, anasema kwamba TASAF imekuwa mkombozi wake kwani inamuwezesha kuendesha maisha bila wasiwasi.

" Kipato kutokana na ajira ya muda kiliniwezesha kupata mtaji wa kuanzisha shughuli ya kupasua kokoto, ambapo ninauza tipa moja kwa shilingi 80,000/= na maisha yanasonga." Anasema Bi. Alibina.

Mnufaika mwingine ni Rahabu Musa Samaki ajira ya muda imemuwezesha kuanzisha mradi wa ufugaji kuku na kupata kipato cha kumuwezesha kusomesha watoto wake wawili hadi Sekondari na wawili ngazi ya stashahada, pamoja na kujenga nyumba ya vyumba vitatu kwa tofali za kuchoma.

**a) Mafanikio**

(i) Ugawaji wa taulo za kike zaidi ya 8000 kwa Wasichana waliopo shuleni kupitia AGYW**;**

(ii) AGYW imesaidia kutoa ruzuku kwa wasichana waliopo shuleni kwa ajili ya mahitaji yao (daftari, sare za shule, kalamu n.k);

(iii) Mafunzo kwa wasichana balehe na wanawake vijana 438 waliopo nje ya shule kupitia AGYW kuhusu namna ya kuandaa maandiko ya biashara;

(iv) Kaya 130 za walengwa zimejiunga na huduma za Mfuko wa bima ya Afya ulioboreshwa (**iCHF)**;

(v) Wanufaika wameanzisha shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, mifugo na biashara ndogo ndogo ili kujiongezea kipato na hivyo kujikwamua kiuchumi;

(vi) Mpango umsaidia kuboresha mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki kwa walio chini ya miaka mitano.

**b) Changamoto**

(i) Idadi kubwa ya wasichana balehe na wanawake vijana kupenda matokeo ya haraka na hivyo kukimbilia kuolewa au kutafuta kazi za ndani badala ya kuandaa maandiko ya biashara ili wapatiwe mitaji;

(ii) Uhitaji mkubwa wa mpango wa AGYW kwa wasichana balehe na wanawake vijana walio nje ya mpango wa TASAF katika vijiji na mitaa ambayo haijafikiwa na mpango;

(iii) Baadhi ya Walengwa wa Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini kutumia fedha za ruzuku kinyume na malengo yaliyokusundiwa kama vile ulevi;

(iv) Kuchelewa kuanza utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizo katika mpango, kama vile ajira za muda mfupi, uboreshaji wa miundombinu ya afya, elimu, barabara, maji na mafunzo ya ujasiriamali.

### 2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri ya Singida ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, yapo mambo kadhaa ambayo yalibainika ikiwa ni pamaoja na Mafanikio na Changamoto.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Singida, ilifanikiwa kufanya urasimishaji wa biashara  za Wafanyabiashara **777** wa Halmashauri ya Singida na kuwajengea uwezo kwa lengo la kuwawezesha biashara zao kuwa kwenye Mfumo rasmi na  unaotambulika Kisheria.

Aidha, pande hizo mbili zimejenga Kituo kimoja cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara (**One Stop Business Formalization and Development Centre**) kwa ajili ya kusaidia urasimishaji wa biashara kuwa wa haraka na wa gharama nafuu kwa mfanyabiashara. Kituo hicho kinawaleta pamoja wadau mbalimbali ili kumuwezesha mfanyabiashara kupata huduma zote muhimu anazozihitaji pale anapotaka kuanzisha biashara yake. Wadau hao ni pamoja na BRELA, TRA, Benki za CRDB na NMB, NSSF, SIDO, TCCIA, NIC na NHIF.

**Mheshimiwa Spika, jengo linalotumiwa kwa kituo hicho awali lilikuwa** ukumbi wa Manispaa ya Singida lakini baada ya pande mbili hizo kuona umuhimu wa kuwa na kituo cha aina hiyo, walikubaliana kubadili matumizi ya ukumbi huo kuwa kituo cha urasimishaji biashara kwa kufanya ukarabati uliogharimu **shilingi milioni 17.3** ambazo zilitolewa na MKURABITA na Manispaa iliweka uwekaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ada na leseni.

Aidha, MKURABITA ilichangia vitendea kazi kwa ajili ya kuwezesha shughuli za urasimishaji kutekelezwa kwa ufanisi kwa kutoa Kompyuta moja, UPS, Scanner na Printer vyote vikiwa na thamani ya **shilingi milioni 4.**

**a) Mafanikio**

i. Kituo kimesaidia kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara kwa kuwawezesha kupata huduma za urasimishaji na uendelezaji biashara katika sehemu moja;

ii. Kuongezeka kwa mapato yanayotokana na ada za leseni ambapo tangu kuanzishwa kwa kituo hicho Disemba, 2019 hadi machi 2020 jumla ya shilingi milioni **52.3** zimekusanywa

iii. Ongezeko la Wafanyabiashara wanaofungua akaunti katika benki ya NMB;

iv. Wafanyabiashara 47 wamenufaika na mikopo yenye thamani ya **shilingi milioni 188** kutoka benki ya NMB na hivyo kuongeza mitaji ya biashara zao;

v. MKURABITA imeingia makubaliano na NMB ili wafanyabiashara **50** waliorasimishwa na MKURABITA katika Halmashauri waunganishwe **NMB Business**

**Clubs** kwa ajili ya kuwapa mafunzo, mitaji na kuunganishwa na masoko;

b) **Changamoto**

i. Uhaba wa Watumishi wa kutoka kwenya Taasisi zinazohudumia kituo kwa muda wote;

ii. Wananchi wengi hawajapata elimu ya kutosha kuhusiana na shughuli na umuhimu wa kituo cha pamoja cha urasimishaji na uendelezaji wa biashara; na

iii. Huduma kutolewa kituoni hapo kwa siku chache (siku mbili) kwa wiki jambo linalowanyima wafanyabiashara wengi fursa ya kupata huduma za kituo.

### 2.2.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma, kilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali tarehe 17 Agosti,2000 baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili; Chuo cha Watumishi wa Serikali kilichokuwa Dar es Salaam (Civil Service Training Centre) na Chuo cha Uhazili Tabora (Tabora Secretarial College). Kwa sasa chuo kina kampasi sita (6) Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya, Tanga, Tabora na Singida.

**Mheshimwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma kampasi ya Singida kilianza rasmi mwezi Julai, 2011 na kilipata usajili kamili wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) wenye **Na.REG/BTP/038** mnamo mwezi Novemba, 2014. Chuo kinaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya cheti na stashahada.

Katika ziara ya ukaguzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida Kamati ilibaini yafuatayo:-

**(a) Mafanikio**

i. Chuo kimefanikiwa kudahili wanafunzi 1,380 tangu kilipoanzishwa;
ii. Chuo kimeweza kujiendesha kwa kutumia mapato ya ndani;
iii. Chuo kimefanikiwa kununua eneo lenye ukubwa wa ekari 76 katika eneo la Mungumaji, Kitongoji cha Sasu

**(b) Changamoto**

i) Chuo hakina majengo yake na hivyo kulazimika kukodi majengo kwa mtu binafsi na hivyo kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kulipa kodi;
ii) Chuo kinakabiliwa na upungufu wa Watumishi wa kudumu na hivyo chuo kutumia fedha za mapato ya ndani kulipa watumishi wa muda;
iii) Ukosefu wa hostel kwa wanafunzi;
iv) Upungufu wa vitendea kazi na samani za ofisi.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inapenda kutoa maoni yafuatayo:-

(i) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia wasichana balehe na wanawake vijana (Adolescent Girls and Young Women – AGYW) kujipatia taulo za kike;

(ii) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia kuboresha maisha ya wanufaika kwa kuwawezesha kumudu gharama mbalimbali za maisha;

(iii) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia kuboresha mahudhurio ya watoto shuleni na katika vituo vya afya;

(iv) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechochea utamaduni wa kaya maskini kujiwekea akiba na kupata elimu ya masuala ya fedha na uendeshaji wa biashara ndogondogo;

(v) Kituo cha Pamoja cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara kiwezeshwe kuwa na wataalamu siku zote za kazi ili kiweze kuhudumia wafanyabiashara muda wote;

(vi) Bajeti finyu ya maendeleo kwa MKURABITA inaathiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji;

(vii) Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida kujenga majengo yake katika eneo la Mungumaji na hivyo kuokoa gharama zinazotumika kwa ajili ya kodi ya pango;

(viii) Serikali ikipatie Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida Watumishi wa kudumu na Vitendea kazi ili kuboresha utendaji na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**,uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa.

Njia zilizotumiwa na Kamati wakati wa uchambuzi huu ni pamoja na kuangalia hali halisi ,kwa kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

### 3.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba Njia kubwa zilizotumiwa wakati wa uchambuzi huu ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa Vikao vya Kamati.

(i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa Fedha (cash flow plan);

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo (Matumizi ya kawaida asilimia **70.98** na Maendeleo asilimia **44.85**);na

(iii) Fedha hazipatikanaji kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa Fedha zilizopokelewa na mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka hazina hadi kufikia mwezi Februari ,2020 (robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,**uchambuzi zaidi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari,2020 Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na mafungu yaliyo chini yake ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 432,987,967,686/=** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Maendeleo kiasi hicho ni sawa na asilimia **63.35** ya Fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge.
Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa takribani **Shilingi 58,281,023,829/=** sawa na Asilimia **15.55** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambacho kilikuwa ni **Shilingi 374,706,943,857/=**

Kwa upande wa fedha za Maendeleo uchambuzi umeonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari,2020,Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora na mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya **Shiling**i **89,646,053,464.88/=** kutoka hazina sawa na asilimia **44.85** ya fedha yote iliyodhinishwa na Bunge kwa ajili ya Maendeleo.
Kiasi hicho cha fedha kimeongeeka kwa **asilimia 9.25** ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambacho kilikuwa **Shilingi 82,052,427,230/=**

Aidha Uchambuzi umebaini kwamba jumla ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani asilimia **63.35** ya fedha zote zilizoidhinishwa .Kwa hali ya kawaida kiasi ambacho kilipaswa kiwe kinaenda asilimia **25** ya kila robo ya mwaka wa fedha hakikuweza kupatikana. Kwa kuzingatia kiasi cha fedha kwa kipindi hicho cha fedha zilizoidhinishwa kilipaswa kuwa kimepatikana na kutolewa kwa takribani **asilimia 75.**

Vile vile, katika kipindi hicho jumla ya **Shilingi 343,341,914,222/=** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **70.98** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo.

Kiasi cha fedha kilichopokelewa kimeongezeka kwa asilimia **17.32** ikilinganishwa na **Shilingi 292,654,516,627/=** zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi kama hicho katika mwaka wa Fedha **2018/2019** .
Hali hiyo inaonesha kuwa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kinachotolewa na Hazina kimeendelea kuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Mwenenndo huu umeshuhudiwa katika miaka minne ya fedha mfululizo tangu mwaka 2016/17 hadi 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina siyo mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani kiasi kinachotolewa kimeendelea kupungua huku upande wa fedha za maendeleo ukiathirika zaidi ikilinganishwa na upande wa matumizi ya kawaida.

3.3 **Mapitio ya Utekelezaji wa** Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**,wakati wa kupitia na kuchambua bajeti Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kwaka 2019/2020 . Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo kumi na tatu **(13)** kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais ,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na Ushauri wa kamati na inaendelee kuzingatia yaliyosalia .Baadhi ya Maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu:-

(i) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi iendelee kutoa mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwakumbusha juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima. Mafunzo hayo yameendelea kutolewa na matunda yake yameanza

kuonekana ambapo vitendo vya ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji vimepungua; na

(ii) Zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika. Zoezi hili limefanyika kwa umakini na kukamilika ambapo kaya zilizoondolewa ni zile zisizo na sifa.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyasisitiza ili Serikali iyatekeleze kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji. Baadhi ya maoni na ushauri hivyo ni pamoja:-

(i) Serikali iongeze mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Serikali haijaongeza Mshahara kwa watumishi wa umma kwa miaka mitatu ya fedha iliyopita; na

(ii) Serikali iongeze bajeti ya maendeleo ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa ardhi na biashara za Wananchi. Hadi mwezi Februari, 2020 MKURABITA ilikuwa haijapokea fedha yoyote ya maendeleo kati ya shilingi bilioni 1.5 zilizoidhinishwa na Bunge.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2020/2021,kwa Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora unajumuisha Mafungu Nane (04,09,20,30,32,33,67 na 94,) na Umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa miaka Mitano (2016/17 -2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015,Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla Ofisi hii pamoja na Mafungu yake imepanga kutekeleza Malengo 174 kwa mwaka ujao wa fedha na Malengo hayo ni haya fuatayo:-

i) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

iii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) na programu za maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

iv) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);

v) Kukarabati majengo ya Ikulu ya Dar es salaam na Ikulu Ndogo za Mwanza, Arusha, Lushoto, Tabora na Shinyanga na Nyumba za Wafanyakazi zilizopo Dodoma;

vi) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino;

vii) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu, na kukamilisha mfumo wa kielekroniki wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III);

viii) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

ix) Kuratibu na kuendesha mikutano sita ya uratibu wa maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

x) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

xi) Kuandaa mkutano wa kimataifa na kikanda na mikutano saba ya kitaifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

xii) Kuendelea na urasimishaji wa Wachimbaji wadogo wa Madini katika Mkoa wa Geita;

xiii) Miradi 2,390, katika sekta ya afya, elimu, maji, ujasiriamali na barabara za vijiji itatekelezwa chini ya mpango wa kutoa ajira za muda katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;

xiv) Kufanya mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na wadau wa Maendeleo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini;

xv) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;

xvi) Kusimamia mikakati ya ukodishaji wa ndege kwa kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL);

xvii) Kupokea matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma

xviii) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo ya kiutumishi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazi;

xix) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 1,115;

xx) Kuendesha mafunzo kwa njia ya mtandao ili kusaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kutoa fursa ya kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi, kupunguza safari nje ya mahali pa kazi na kuepuka kuwa mbali na familia;

xxi) Kusanikisha katika taasisi za umma, Mfumo Shirikishi wa Kusimamia shughuli za Rasilimali za Taasisi;

xxii) Kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa;

xxiii) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

xxiv) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira kwa ajiri za Muungano;

xxv) Kufanya mikutano ya Kisheria ya Tume ili kujadili na kutolea uamuzi rufaa na malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

xxvi) Kufanya utafiti kuhusu mazingira magumu ya kazi;

xxvii) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za Umma, taasisi na watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ,inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 699,956,320,000**.Kati ya fedha hizo **Shilingi 517,131,499,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na **Shilingi 182,824,821,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.
Aidha,Katika fedha za matumizi ya kawaida **Shiling**i **39,154,604,000** sawa na **asilimia 5.58** ni Kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 477,976,895,000/=** sawa na asilimia **68.29** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba,bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa **Shilingi 16,427,108,383**/= sawa na asilimia **2.4** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ilikuwa **shilingi 683,529,211,617/=.**

Aidha ,kwa upande wa wa Fedha za Matumizi ya kawaida katika mwaka ujao wa fedha zimeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **33,469,533,000/=** ambacho sawa ni asilimia **6.92** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2o19/2020 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa **Shilingi 483,661,966,000/=.**

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kiasi cha Fedha za Miradi ya Maendeleo kinachoombwa kimepungua kwa **Shilingi 17,042,434,617/=** sawa na Asilimia **8.53** ilinganishwa na fedha za miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha **2019/2020** ambacho zilikuwa Shilingi **199,867,255,617/=**

## 4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,**Uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Uchambuzi umelenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

(i) Bajeti ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo ni **Shilingi 699.56** ni sawa na asilimia **2.01** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2020/2021 ni **Shilingi 34,876/=**

(ii) Mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 unaonesha ongezeko la bajeti kwa **asilimia 5.36** ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa 2019/2020 wakati Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imeongezeka kwa **asilimia 2.4** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020; na


(iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia **5.3** katika fedha za Maendeleo ambazo ni sawa asilimia **36.98** ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021; Hili hali bajeti ya Maendeleo ya ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora ambayo ni sawa na asimilia 2.01 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa Asilimia **2.4** ikilinganisha na Mwaka wa fedha 2020/2021.

**Jedwali Na. 1:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021


| **BAJETI KUU YA TAIFA 2020/2021** | | | **BAJETI YA OFISI YA RAIS UUB 2020/2021** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mgawanyo** | **Bajeti Kuu (Tsh. Milioni)** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti Kuu** | **Mgawanyo** | **Bajeti ya Wizara** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara** |
| OC | 3,741,137 | 10.73 | OC | 477,976,895,000 | 68.29 |
| Deni la Taifa | 10,476,834 | 30.4 | - | - | - |
| Mishahara | 7,762,389 | 22.25 | Mishahara | 39,154,604,000 | 5.59 |
| Maendeleo | 12,899,433.8 | 36.98 | Maendeleo | 182,824,821,000 | 26.12 |
| **Jumla** | **34,879,793** | **100** | **Jumla** | **699,959,320,000** | **100** |

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB kwa Mwaka wa fedha 2020/2021**.**

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-




**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20




**Chanzo:** Randama ya OR – UUB kwa Mwaka wa fedha 2020/2021

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ,taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha,Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iangalie namna ya kutatua Changamoto ya upungufu wa watumishi wa umma haswa wa kada za Afya na Elimu ambayo kwa sehemu kubwa imechangiwa na watumishi wengi kuondolewa kazini baada ya kubainika kutumia vyeti vya kughushi;

(ii) Serikali iongeza mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka mara kwa mara. Aidha, hali hiyo imechangia watumishi kukosa ari ya utendaji na kuishia kulalamika kuwa maisha yamekuwa ghali;

(iii) Serikali ichukue hatua ili kuondoa ucheleweshaji wa Watumishi wa Umma kupanda madaraja na kubadilishiwa Mishahara, hali ambayo

imesababisha baadhi yao kustaafu bila kupata stahiki na haki zao. Aidha hali hiyo inasababisha maumivu kwa watumishi hao na baadhi yao kutafsiri kwamba, wanadhulumiwa na Serikali stahiki na haki zao;

(iv) Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali kupitia Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU ) za kushughulikia Rushwa kubwa ambapo watuhumiwa wamekamatwa na kushitakiwa kwenye vyombo vya Sheria.Hata hivyo Kamati inashauri juhudi zaidi ziongezwe hasa katika kupambana na Rushwa ya Ngono ambayo imekuwa ikilalamikiwa kushamiri katika Taasisi za Elimu,Sehemu za kazi na maeneo mengine ya jamii;

(v) Serikali ihakikishe halmashauri zinawatumia kikamilifu Maafisa Maendeleo ya Jamii, na Maafisa Ustawi wa jamii kwa ajili ya kuwaelimisha na kuwasimamia wanufaika wa mpango wa ruzuku wa kaya maskini ili kuhakikisha wanaelekeza sehemu ya ruzuku wanazopata kwenye shughuli za kiuchumi ili kuondokana na umaskini;

(vi) Serikali ihakikishe inatumia kikamilifu fedha ilizozipata kwa ajili Utekelezaji awamu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kuyafikia maeneo yote yaliyobaki ( Vijiji/Mtaa/Shehia 5,693) ili kuwapa wananchi wa maeneo hayo fursa ya kunufaika na mpango;

(vii) TASAF iongeza wigo kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya Kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki), ili kuharakisha na kurahisisha malipo kumfika mlengwa moja kwa moja. Aidha, mfumo huo utasaidia kuondoa malalamiko kutoka kwa baadhi ya walengwa kwamba wamekuwa hawapati malipo kamili yanayostahili;

i) Serikali iongeze kiasi inachochangia katika utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, kwani bado mchango wake ni mdogo sana. Tangu mpango huu ulipoanza mwaka

wa fedha 2013/2014, hadi taarifa hii inaandaliwa Serikali imechangia **shilingi bilioni 8.12** tu kati ya **shilingi bilioni 70** ilizopaswa kuchangia, sawa **asilimia** 11.58. kwa ufafanuzi ufuatao: -

**Jedwali Na. 02:** Mchango wa Serikali na kiasi ilichotoa

| Na. | Mwaka wa Fedha | Kiasi kilichoahidiwa (Tshs. Bilioni) | Kiasi kilichotolewa (Tshs. Bilioni) | Bakaa (Tshs. Bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 01. | 2013/14 | 18.50 | 3.00 | 15.50 |
| 02. | 2014/15 | 14.00 | 0.00 | 14.00 |
| 03. | 2015/16 | 14.00 | 0.60 | 14.00 |
| 04. | 2016/17 | 14.00 | 0.00 | 14.00 |
| 05. | 2017/18 | 3.00 | 0.75 | 2.25 |
| 06. | 2018/19 | 3.00 | 3.00 | 0.00 |
| 07. | 2019/20 | 3.5 | 1.01 | 2.5 |
| | **Jumla** | **70** | **8.12** | **61.91** |

(viii) Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinashirikiana na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania **(MKURABITA)** ili ziweze kuanzisha **(One Stop Business Formalization and Development Centre**) kwa ajili ya kusaidia kurahisisha urasimishaji na uendelezaji wa biashara kwa kupunguza gharama na muda;

(ix) Serikali ihakikishe Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatoa mafunzo kwa Viongozi wa Umma wanaoteuliwa katika nyadhifa mbalimbali kabla hawajaanza kutekeleza majukumu yao. Hali hii itasaidia kuwakumbusha Viongozi hao kuzingatia maadili ya kiutendaji, kujiepusha na mgongano wa maslahi na kuishi kwa kuzingatia kiapo cha ahadi ya uadilifu;

(x) Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utumishi wa Umma kujenga majengo yake katika eneo la Mungumaji – Manispaa ya Singida ili kuwezesha Kampasi ya Singida kuwa na majengo yake na hivyo kuokoa gharama nyingi zinazotumika kwa ajili ya kulipa kodi ya pango.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi mkubwa.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa Taarifa hii. Kwa kutambua kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati katika Bunge hili la Kumi na Moja, nitumie fursa hii kuwatakia Wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge wengine wote kila lakheri katika uchaguzi ujao na Mwenyezi Mungu atujaalie turejee sote katika Bunge lijalo ili tuendeleze gurudumu la ujenzi wa Taifa letu kwa kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuwakilisha wananchi na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inashughulikia mafungu ya bajeti 36 ambayo ni mengi kuliko Kamati nyingine ya Bunge, na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na wakati mwingine hadi jioni kabisa. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa namna yoyote ile kwa Wajumbe kutekeleza jukumu la

uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara tosha ya utayari wa Wabunge kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb
5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba,Mb
7. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
8. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb
9. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate,Mb
10. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
11. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum,Mb
12. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
13. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
14. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb

19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
25. Mhe. Mansoor Hirani Shanif, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Laurean Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt. Fransic Michael kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao na utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndg. Gerlad Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima, Ndg. Asmin Kihemba na Ndg. Prosper Minja wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S. Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU**
**YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**

15 Aprili, 2020